KUTOKA KITABU CHA "MALEZI DONDOO 24" kilichoandikwa na mwandishi Alphonce Cosmas Luhamba

NAMNA YA KUKUZA UBUNIFU KWA WATOTO NA VIJANA.

Hivi karibuni nimezindua kitabu cha, **"Malezi, Dondoo 24"** kitabu ambacho kimesheheni dondoo mbalimbali muhimu kwa walimu, wazazi na walezi. Dondoo hizo zinahusu usalama wa watoto, vyanzo vya tabia, mfumo wa motisha, kuwazuia watoto na vifaa vyenye kutoa mwanga, ufahamu kuhusu ubongo wa mtoto, ukuaji wa watoto, ubunifu na umuhimu wa baba na mama kuhusika kwa pamoja katika malezi. Kitabu cha **"Malezi, Dondoo 24"** kimeelezea kwa lugha rahisi ambayo kila mzazi anaweza kuelewa. Moja ya mambo ambayo kitabu kimetilia mkazo ni mfumo wa elimu na mazingira ambayo yanakuza ubunifu wa mtoto. Katika makala hii nitajikita na dondoo ya 17 kati ya 24 zilizopo katika kitabu. Dondoo ya 17 inahusu ubunifu wa watoto.

Watoto wanatumia sana upande wa kulia wa ubongo, upande ambao unasifa ya kufanya kazi vizuri kwenye mazingira ambayo hayana makatazo, sheria na kanuni. Sehemu hiyo ya ubongo inafanya kazi kwa ufanisi katika uhuru. Ile acha hiki acha kile inamfanya mtoto kupungua katika uwezo wake wa ubunifu.

Tunafahamu N.A.S.A ni taasisi ya nchini Marekani ambayo inahusika na program za usimamizi na uratibu wa mambo ya anga za mbali (space). Mwaka 1960 shirika hilo (N.A.S.A) walianza utafiti wa kipekee, waliazimia kutokwenda anga za mbali badala yake kuzama anga za ndani za ubunifu wa binadamu. Walitaka kuwabaini watu wenye akili za ajabu kwa ajili ya mradi wao wa kwenda anga za mbali. Kazi hii ilikuwa chini ya George Land na timu yake. Walifanya zoezi lao kwa kuwachukua watoto watano wenye umri wa miaka 3 hadi miaka 5. Kabla ya kuanza shule ujiniazi na ubunifu ndani ya watoto hawa ulikuwa wastani wa 98%. Kipimo kilihusisha ubunifu wao, uwezo wao wa kutatua matatizo na ujiniazi wote ndani ya watoto. Cha ajabu ni kwamba hitimisho lao lilionesha kuzorota na kushuka kwa ubunifu, kupungua uwezo wa kuona mbali na kutatua matatizo kulisababishwa na mfumo wa elimu.

Hayati George Land alichunguza na kubaini kwamba, ubunifu hupungua sana kutoka 98% utotoni hadi 30% mtu anapofika umri wa miaka 10 na hadi 12% katika miaka 15 na mwishowe ubunifu hubaki 2% katika utu uzima.



ISBN 978-9987-404-17-9

+255622334199 / +255766006040
alphonceluhamba@gmail.com
Alphonceluhamba
@c_alphonce

Utafiti huu wa bwana George Land ulibaini ubunifu huu umepungua kutokana na mfumo wa elimu. Ndio maana ubunifu hushuka kwa kasi siku za mwanzoni za mtoto anapokwenda shuleni. Mifumo ya elimu haikuzi ubunifu na utatuzi wa matatizo.

Inasikitisha kwa sababu George Land anasema watoto wanakwenda shule ili kujifunza namna ya kutokuwa wabunifu na maisha ya fikra dumavu zisizo na ubunifu yaani, "going to school to learn uncreative behavior and thinking"

Watoto wanapoteza sehemu kubwa ya ubunifu wanapoanza shule, Utafiti wa NASA unaonesha shule inadidimiza ubunifu kutoka 98% hadi 2% ya kusanyiko la watoto wenye akili za hali ya juu waliofanyiwa utafiti. Sheria, mitaala na utaratibu wa baadhi ya shule huua ubunifu na kuwafanya watoto kukosa uhuru wa kuonesha vipaji na ujasiri ambao Mungu amefungasha ndani yao. Mtoto anabaki kuwa mtoto na katika umri wa miaka 1-5 mtoto anastawi sana katika mazingira yenye uhuru pasipo na makatazo mengi.

Mtoto atapiga kelele, atachana karatasi na kuvunja vitu. Jukumu la walimu ni kumlinda na kumsaidia na si kuweka makatazo na kumpiga viboko. Mtoto ni kama sanduku/furushi la zawadi, kazi ya walimu na walezi ni kulifungua taratibu na si, kupandikiza au kuumba kilichomo ndani ya sanduku. Elimu ni mchakato kuwezesha mtu kujifunza kukabiliana na mazingira yake. Kwa watoa elimu wanabaki kuwa wawezeshaji muhimu wa kumsaidia mtoto kuwa vile alivyo. Utafiti wa George Land unasikitisha kwa mtoto aliyezaliwa na IQ kwa asilimia 98% kushuka hadi 30% anapofika miaka 10 kwa sababu ya mifumo ya elimu isiyokuza ubunifu na utofauti. Maja ya mambo ambayo huzuia watu wabunifu kufikia kilele cha maisha yao ni ile hali ya kulazimishwa kufanana na wengine au kulazimishwa kuendana na kilichopo.

Kama ambavyo nimesisitiza hapo juu, mtoto anamatumizi makubwa sana ya ubongo wa kulia, kipande hicho cha ubongo hakifurahii sana mazingira ya sheria na kanuni. Ustawi wa mtoto ni katika uhuru na si katika mfululizo wa sheria. Zamani watoto tuliruhusiwa kucheza kwa uhuru, ukiitwa ulikuwa unajua chakula kimeiva na si vinginevyo. Shule ya IBM (IBM creativity school) inapendekeza njia zifuatazo ili kukuza ubunifu:



ISBN 978-9987-404-17-9

+255622334199 / +255766006040
alphonceluhamba@gmail.com
Alphonceluhamba
@c_alphonce

I. **Kuruhusiwa kukosea na kushindwa (Permsion to fail)-**Ubunifu unakuzwa kwa kuweka mazingira yanayoruhusu kujaribu na kushindwa. Ili kukuza ubunifu ni muhimu mazingira yawaruhusu watoto kukosea, kuna somo muhimu katika majaribio ambayo hayatafanikiwa;

II. **Kuhusiana na taasisi/marafiki wenye akili na ubunifu wa hali ya juu:-** Ukizungukwa na watu bora itakupa nafasi na wewe kuwa bora. Mzazi mjengee mwanao ukaribu na watu wenye fikra bunifu, awaepuke watu wa wastani yaani, watu wa daraja "C" maarufu kwa lugha ya kigeni mediocre;

III. **Kufuata mchakato wa kuondoa maarifa ya zamani kichwani**(unlearning process):-Fikra dumavu na zisizo za kibunifu zinafundishwa shuleni, ndio maana watoto walipoanza shule ubunifu wao ulipungua kutoka 98% hadi 30% walipofika miaka 10. Kwa hiyo ili uwe mbunifu ni muhimu ufute na kuachana na maarifa ya kizamani yanayotolewa shuleni;

IV. **Kuachana na mitindo iliyopitwa na wakati inayopendekezwa na elimu ya sasa:-**Kwa mujibu wa George Land elimu hii ya kukariri na kufanya mitihani ya kufanana ni chanzo cha kuua ubunifu. Tuwe na mafunzo na mitaala inayokuza ubunifu kwa watoto;

V. Kujitambua:- Je, tunaweza kuamini katika ndoto kubwa kupitiliza yaani, crazy dreams ambazo watoto wanawaza kuhusu kesho yao? Ni muhimu kupambana na mipaka ambayo mila na desturi zimeweka juu yako na watoto wako. Kujitambua ni pamoja na kujua mipaka ya kijamii ambayo umewekewa kama pingu ya kuzuia mafanikio. Mtoto ajengewe uwezo ili avunje miiko na mipaka yote ya mafanikio. Mpaka si jambo dogo, ni kizuizi ambacho vizazi vingi vimekikubali na kukiheshimu. Mzazi hakikisha mijadala isiwe na kinga nyumbani kwako, watoto wako wapewe taarifa sahihi, wasizuiwe kujadili mambo muhimu. Mtoto asizuiwe kuota ndoto yoyote akiwa macho, atafikiaje hiyo ndoto? Hatujui, lakini hatumlazimishi awaze kama wengine wanavyowaza. Tujenge kizazi ambacho mtoto halazimishwi kufanana na wenzake kifikra. Mtoto akiwezeshwa kujitambua atailinda akili yake.



ISBN 978-9987-404-17-9

+255622334199 / +255766006040
alphonceluhamba@gmail.com
Alphonceluhamba
@c_alphonce

Moja ya sababu ya kutokutazama picha za ngono ni kwa sababu akili ni sehemu takatifu ya mwili yaani, sacred place of reasoning na inapaswa kulindwa. Kupitia akili watu wamebuni chanjo zikaleta kinga dhidi ya magonjwa, kwa akili watu wamebuni sera zilizokuza uchumi na kuleta majawabu, kwa akili na ufahamu watu wamefanya tafiti zenye kuongeza uzalishaji.

Uchambuzi huu unaletwa kwenu na, **Alphonce Cosmas Luhamba**

Namba ya Simu unaweza kuagiza nakala yako ya kitabu, **0656090300**



ISBN 978-9987-404-17-9

+255622334199 / +255766006040
alphonceluhamba@gmail.com
Alphonceluhamba
@c_alphonce